SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WAFANYAKAZI TANZANIA

(TUCTA)

RISALA YA WAFANYAKAZI KATIKA MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA MEI-MOSI KITAIFA

UWANJA WA JAMHURI
MOROGORO

MEI 2023

- Ndugu Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Dkt. **Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
- Mheshimiwa **Kassimu MajaliwaMajaliwa**(Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
- Mheshimiwa **Tulia Ackson,** (Mb) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
- Mheshimiwa **Profesa Joyce Ndalichako** (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira Vijana na Watu wenye Ulemavu,
- Ndg**. Tumaini Nyamhokya,** Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania, (TUCTA),
- Viongozi Wakuu wa TUCTA,
- Wenyeviti na Makatibu Wakuu wa Vyama Shiriki – TUCTA,
- Mhe**. Fatma Mwasa**, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,
- Ndugu **Wellington Chibebe,** Mwakilishi wa Shirika la Kazi Duniani,
- Mheshimiwa **Dr. Yose Miyambina,** Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi,
- Mheshimiwa **Ms Suzan Mkangwa,** Kamishna wa Kazi
- Mheshimiwa **Pendo Berege,** Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri,
- Mheshimiwa **Jayne Nyimbo,** Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE),
- Ms**. Suzan Ndomba**, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE),
- Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri,
- Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara,
- Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya mliopo hapa,
- Waheshimiwa Mabalozi,

- Waheshimiwa Wabunge,
- Viongozi wa Vyama vya Siasa mliopo hapa
- Wanachama wa vyama vya wafanyakazi na Wafanyakazi wote
- Viongozi wa Dini
- Wanahabari,
- Mabibi na Mabwana,
- Itifaki imezingatiwa.

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Naomba nitumie fursa hii adhimu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutukutanisha tena leo baada ya kipindi cha mwaka mmoja kupita kwenye tukio kama hili pale Dodoma.

Aidha, tunamshukuru Mungu kwa kukupatia kibali na kukusafirisha wewe na wageni wengine wote pamoja na wafanyakazi kwa salama na hivyo kuweza kushiriki sherehe hizi za mwaka 2023. Karibu sana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Maadhimisho ya Mei Mosi mwaka huu 2023 yameratibiwa na vyama Vyote Shiriki kupitia TUCTA**.** Shukrani za dhati ziende kwa vyama vyote kumi na vitatu vinavyounda Shirikisho ambavyo ni; - **DOWUTA**, **TUICO, TAMICO, CWT, RAAWU, TUGHE, COTWU (T), TEWUTA, TALGWU, TPAWU, CHODAWU, TASU,** na **TRAWU** kwa mshikamano waliouonesha. Aidha katika sherehe

za mwaka huu, vyama vya wafanyakazi vilivyo nje ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA)vimeshiriki pia.

Kwa namna ya pekee sana niwashukuru sana wadau wote walioshirikiana nasi kuhakikisha kuwa sherehe hizi zinafanikiwa sana. Niushukuru sana uongozi wa mkoa wa Morogoro chini ya Mkuu wa Mkoa wetu mahiri Mheshimiwa Fatma Mwasa pamoja na wasaidizi wake wote kwa jinsi walivyoipokea na kushughulika na shughuli hii. Mkuu wa Mkoa alitupokea kwa moyo mmoja na aliibeba shughuli hii kwa mikono miwili na ndio maana imefanikiwa na kufana sana.

Shukrani za dhati kwa Mh. Waziri wetu wa Kazi Komredi Profesa Joyce Ndalichako pamoja na timu yake yote kwa jinsi walivyoshirikiana nasi kwenye maandalizi na hatimaye kilele cha sherehe hizi.

Pia nimshukuru Mdhamini wetu Mkuu CRDB Bank Limited, Wadhamini wetu; NMB Bank, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mifuko ya hifadhi ya jamii ya NSSF na PSSSF, pamoja na Wadhamini wengine wote ambao kwa michango mbalimbali wamewezesha shughuli hii kufanikiwa sana.

2.0 SHUKURANI

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa niaba ya wafanyakazi wote nchini, TUCTA inatoa shukurani za pekee kwako kwa kupokea na kukubali mwaliko wa kuwa Mgeni Rasmi katika sherehe hizi. TUCTA inaelewa wingi wa majukumu uliyonayo na huenda isingekuwa rahisi kwako kukubali mwaliko huu, lakini umeendelea kutambua thamani ya kundi hili muhimu la wafanyakazi nchini na umekubali kushiriki nasi. Aksante sana mama.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Tunapenda kukujulisha kuwa sherehe hizi zilitanguliwa na shughuli mbali mbali za awali kuelekea siku ya kilele. Tunafurahi kukujulisha kuwa tulianza na Michezo kwa wafanyakazi ambapo timu 31 zimeshiriki michezo mbalimbali ili kutimiza suala la afya kwa wafanyakazi. Pia wafanyakazi ambao ni machinga, Bodaboda, wasanii na wafanyakazi wa taasisi mbalimbali walishiriki kusafisha masoko ya Mawenzi na Kingalu na kupanda miti kwenye vyanzo vya maji ikiwa ni mwanzo wa lengo la kupanda miti milioni mbili. Aidha, maonesho ya OSHA chini ya Wakala wa Afya na Usalama Mahala pa kazi Tanzania yalifanyika ambapo jumla ya taasisi themanini zilishiriki. Tulifanikiwa pia kwa mara ya kwanza kuanzisha TUCTA Mei Mosi Marathon ambapo wakimbiaji takribani 1500 walishiriki mbio hizo. Shughuli hizi zote zilileta hamasa kwa wafanyakazi

na kuongeza ushiriki wa wanachi kwenye sherehe hizi na pia kuleta chachu kwa wanachi wa Morogoro.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Sisi wafanyakazi tukiwa ni miongoni mwa wanajamii wa Tanzania, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kukusimamia na kukupa nguvu na weledi katika kutuongoza kwa nafasi yako kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka miwili sasa. Wote tumeendelea kushuhudia hatua kubwa ambazo nchi yetuimezipiga katika kipindi hiki cha uongozi wako katika Nyanja mbalimbali.

Sisi wafanyakazi tumekuwa ni miongoni mwa wanufaika wakubwa wa matokeo ya hatua zako katika kujenga nchi yetu Tanzania Kiuchumi, Kisiasa na kijamii. Kutokana na hatua mbali mbali unazochukua tumeendelea kushuhudia umoja na mshikamano ukiendelea kuimarika miongoni mwa Watanzania bila kujali dini, itikadi za kisiasa wala kabila. Tumeshuhudia utulivu wa kisiasa na kiuchumi kuimarika hasa baada ya kuifungua nchi kibiashara kitaifa na kimataifa. Tunatambua kazi kubwa unayoifanya kwa kusafiri na kutuhangaikia ikiwa ni pamoja na kuwaleta wawekezaji wa kimataifa na hata wageni wengine wa kimataifa kuja nchini kwetu. Ujio wa wageni hawa tunaamini utathibitisha ile kauli ya Mgeni njoo mwenyeji apone.

3.0 KAULI MBIU:

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kauli Mbiu katika Sherehe za Mei Mosi mwaka huu 2023 ni; - **"Mishahara Bora na Ajira za Staha" ni Nguzo kwa Maendeleo ya Wafanyakazi" Wakati ni SASA!"**

Kauli Mbiu hii inaendana na lengo la Wafanyakazi duniani la kufanya kazi ili kupata ujira ambao ni mshahara. Vivyo hivyo sisi wafanyakazi wa Tanzania, Mshahara kwetu ni jambo nyeti ambalo ndio tunabadilishana na waajiri wetu baada ya kutoa nguvu, weledi, uaminifu na ufanisi katika kuhakikisha malengo ya kazi yanatimia. Kwa mantiki hiyo, tunatarajia waajiri wetu kuendelea kutimiza wajibu wao wa kutupatia mishahara bora ambayo tumekubaliana kwenye mikataba. Aidha, mazingira ya kazi zetu kuendelea kuwa salama, rafiki, yenye kujali afya zetu na kutuepusha na hatari zitokanazo na kazi yanasaidia sana kuleta heshima, haki na uhakika kwa wafanyakazi. Endapo Waajiri watatimiza haya yote kwa ukamilifu, ndio yanasababisha uwepo wa ajira zenye staha ambazo ndio nguzo ya maendeleo kwetu wafanyakazi.

Kauli mbiu hii inatukumbusha sote yaani waajiri na wafanyakazi kwa ujumla kuendelea kutekeleza majukumu yetu ili kila mmoja afikie malengo yake kazini. Wafanyakazi tutimize malengo ya mwajiri naye pia atimize wajibu wake kwa wafanyakazi kwa kuwapa malipo stahiki kwa mujibu wa

mikataba na viwango vyote vinavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya kazi.

4. TATHMINI YA MEI MOSI ZA 2021 NA 2022

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Hakuna wakati ujao bila ya wakati uliopo na uliopita. Katika Sherehe zetu za Mei Mosi za mwaka 2021 Mwanza na 2022 Dodoma, wewe ulikuwa mgeni Rasmi kama ilivyo hivi leo. Katika Sherehe hizi mbili, sisi wafanyakazi ulitugusa sana kwa jinsi ulivyozipokea na kuzishughulikia kero zetu mbali mbali tulizowasilisha kwako. Kero zote ulizozipokea, ulizitolea maelekezo na kufanyiwa kazi mara moja. Sisi wafanyakazi tumekuwa ni mashuhuda na wanufaika wa moja kwa moja wamatokeo ya maelekezo yako. Naomba nitumie fursa hii kukumbusha machache tuliyoyawasilisha kwako na umeyafanyia kazi:-

- Nyongeza ya Mishahara kwa Kima cha Chini kwa asilimia 23.3%.
- Kupungua kwa ucheleweshajiwa malipo ya Mafao kwa Wastaafu, ikilinganishwa na hapo awali.
- Kuridhiwa kwa Mikataba ya Hali Bora ya Kazi.
- Kurekebishwa kwa Miundo ya taasisi mbalimbali, ambapo serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina imeendelea kutoa miongozo mbali mbali kuhusu uundaji wa motisha (*Incentive schemes)* na miundo ya taasisi zilizo chini yake.

- Kufanyika kwa maboresho ya Sheria na miongozo mbalimbali ihusuyo Wafanyakazi katika ngazi zote,tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Kwa sasa tunaiona dhana ya ushirikishwaji kwa vitendo.
- Baadhi ya Taasisi kutekeleza kwa ukamilifu dhana ya ushirikishwaji wa Wafanyakazi kupitia Mabaraza ya Wafanyakazi.
- Wafanyakazi walioondolewa kazini kutokana na dosari za Vyeti vyao kulipwa michango yao ya NSSF/PSSSF.
- Kuongeza fursa ya kunufaika kwa watoto wa Mwanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.
- Punguzo la kiwango cha kodi ya mapato ya PAYE toka 9% hadi 8% kwa mishahara ya kima cha chini.
- Kupunguza tozo kwenye miamala ya kifedha.
- Kuondoa tozo ya asilimia 6% ya ada ya kushikilia kwa Wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya juu jambo ambalo lilikuwa ni kero kubwa kwa wafanyakazi vijana wanaotoka vyuo vikuu na hivyo kushusha ari na ufanisi kazini.
- Serikali kuajiri zaidi ya Wafanyakazi 40,000.
- Kupandisha madaraja kwa Watumishi zaidi ya **262,782** ambao pia wamelipwa stahili zao na nyongeza za mishahara yao sawa na jumla ya **Tsh. 58.1B**
- Kuendelea kutekeleza Miradi mikubwa ya kimkakati, ambapo ajira za moja kwa moja zimeongezeka.
- Kuendelea kujenga mazingira rafiki ya Kazi, Uwekezaji na Uzalishaji.

- Ujenzi wa miundo mbinu kwa baadhi ya maeneo ambayo yamerahisisha ufanyaji kazi na hivyo kuongeza ufanisi katika Nyanja mbalimbali.

TUCTA tunashuhudia serikali inavyoendelea kuiishi kauli mbiu yetu kwa kuweka mazingira rafiki kwa wafanyakazi wenzetu hasa waalimu kwa kujenga madarasa ya kisasa, ofisi na nyumba za waalimu. Watumishi wa Afya wameendelea kujengewa majengo mengi mazuri na kupatiwa vifaa na vitendea kazi vya kisasa kabisa na hivyo kusababisha mazingira ya kazi kuwa rafiki na kuvutia. Pia tumeshuhudia maafisa ugani sasa wakipewa pikipiki za kisasa kabisa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa urahisi, tofauti na hapo awali ambapo wengi walifanyakazi katika mazingira magumu sana.

5. KUUNGA MKONO JUHUDI ZA KUPUNGUZA TATIZO LA AJIRA KWA VIJANA NA UBORESHAJI WA HUDUMA YA HIFADHI YA JAMII

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika kuunga mkono juhudi za serikali katika kuongeza ajira kwa vijana, TUCTA kwa kushirikiana na ATE, tumeweza kuandaa mafunzo ya ufundi stadi kwa kozi za umeme wa viwandani na majumbani, utengenezaji wa mitambo ya kupooza (cooling and refrigeration), ukerezaji vyuma na upishi (food production). Mafunzo haya yanafanyika baada ya kufanya utafiti wa mahitaji kutoka kwenye sokoukilinganisha

na wahitimu wa kozi hizo waliopo sokoni. Mafunzo haya yanafanyika kwa kushirikiana na vyama vya waajiri na wafanyakazi wa Denmark. Aidha, mafunzo haya yanafanyika katika vyuo vya VETA; Dar es salaam, Morogorona Mikumi,pamoja na chuo cha Don Bosco chini ya uhakiki ubora wa NACTVET. Mpaka sasa jumla ya wanafunzi 270 wanafadhiliwa katika mafunzo haya ya miezi sita darasani na mwezi mmoja kwenye vitendo. Kwa utekelezaji wa mafunzo haya katika kipindi cha miaka miwili tunatarajia kuongeza nguvu kazi ya vijana wapatao mia nane kwenye soko la ajira nchini.

6. HOJA MBALIMBALI ZA RISALA YA WAFANYAKAZI

6.1 HALI YA MISHAHARA YA WAFANYAKAZI:

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Tunatambua kuwa kwa sasa hali ya uchumi inaendelea kukua taratibu kutokana na changamoto mbali mbali za kidunia na sisi kama nchi hatupo kisiwani na kwamba zinatuhusu pia. Hata hivyo, tunatambua pia jitihada za serikali yako kwa ongezeko la mshahara lililofanywa mwaka jana la asilimia 23.3 kwa kima cha chini ambapo watumishi wa kima cha kati na juu waliguswa kidogo sana.

Sisi wafanyakazi tunaendelea tena kubisha hodi na kuomba uendelee kutukumbuka kwa kutuongezea mishahara inayogusa makundi yote kwani gharama za maisha

zimepanda sana, na hasa ukizingatia wafanyakazi hawa walikaa muda mrefu bila kupandishwa mishahara.

Mheshimiwa mgeni rasmi

Bodi ya kima cha chini Sekta binafsi, ilikutana mwezi Juni, 2022 na kupendekeza kima cha chini cha Mpito (Interim minimum wage) ambacho kilitarajiwa kuanza kutumika mwezi Julai, 2022 sambamba na ongezeko la watumishi wa Sekta ya umma. Hata hivyo, kima cha chini Sekta binafsi kimeanza kutumika mwezi Januari, 2023 baada ya Tangazo la Serikali GN 45 la mwezi Disemba, 2022.

TUCTA tunaiomba serikali kupitia bodi ya kima cha chini ifanye utafiti sawa na matakwa ya sheria ili kupata kima cha chini kilichofanyiwa utafiti.

Mheshimiwa mgeni rasmi

Utumishi wa umma unagusa na kujumuisha mashirika ambayo yanazalisha faida, ambayo ni sehemu ya jitihada za wafanyakazi katika kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na ubunifu. Hivyo, suala la mikataba ya hali bora linalohusu wafanyakazi na kunufaika na matokeo ya juhudi zao ni la muhimu kwani linafanya taasisi hizi kuendelea kuzalisha faida zaidi huku wafanyakazi wakiandaliwa mazingira bora ya kazi na kimaslahi.

Aidha, mfumo wa uidhinishaji wa mikataba hii kwenye utumishi wa umma umekuwa ukichelewa katika hatua mbalimbali hivyo kuondoa maana halisi ya haja ya kuwepo kwa mikataba ya hali bora.

Pamoja na uidhinishaji kugusa Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi na Utawala bora, Tunakuomba uzielekeze taasisi hizi zishughulikie mikataba hii kwa wakati ili kuondoa ucheleweshaji uliopo sasa.

MADAI YA MALIMBIKIZO YA MISHAHARA YA WATUMISHI WA HOSPITALI TEULE ZA MIKOA NA WILAYA (DDH NA CDH)

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Wakati wa mazoezi ya uhakiki wa vyeti vya taaluma kwa Watumishi wa Umma, baadhi ya Watumishi katika Hospitali Teule za Wilaya (CDH) na Mikoa walisitishiwa mishahara yao kwa vipindi tofauti kupisha uhakiki ingawa waliendelea kufanya kazi. Baada ya uhakiki ule kukamilika na wengi wao kuonekana hawana tatizo katika vyeti vyao, mishahara ilirejeshwe na wakaendelea kulipwa kama kawaida lakini hawakulipwa malimbikizo ya mishahara iliyokuwa imesimamishwa kupisha uhakiki. Baadhi ya Hospitali hizi ni pamoja na Murgwanza CDH, Nyakahanga CDH, Isoko CDH, Biharamulo CDH, Bunda CDH, Ilula CDH na nyingine ambazo bado TUCTA tunafuatilia.

Kupitia risala hii, TUCTA tunakufahamisha kuwa, kwa kipindi chote tangu zoezi la kwanza la uhakiki mwaka 2015 hadi leo, Watumishi wa CDH na Watendaji wa kata na vijiji waliosimamishwa na baadaye kurejeshwa kazini wanaodai malimbikizo ya mishahara hawajalipwa licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Vyama vya sekta husika. Tunaomba sasa Serikali ione umuhimu wa kuwalipa Watumishi hawa ambao wamekuwa wavumilivu kwa muda mrefu.

6.2 KODI INAYOKATWA KUTOKA KWENYE MARUPURUPU

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Tunatambua kuwa jukumu la kulipa kodi ni la kisheria ili kuwezesha serikali yetu kuendelea kutekeleza kazi zake ikiwa ni pamoja na kutulipa mishahara. Tunaungana nawe Mheshimiwa Rais kusisitiza kuwa ni lazima kila mfanyakazi alipe kodi. Pia kwa wale wote wanaotakiwa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria walipe kodi zao kikamilifu. Tunawapongeza sana TRA kwa kuendelea kuboresha mifumo yao ya ukusanyaji kodi na kuendelea kubuni vyanzo vipya vya makusanyo kila mwaka kama wanavyoelekezwa na Wizara yetu ya Fedha na Mipango na kuidhinishwa na Bunge letu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Pamoja na punguzo la kodi ulilotupatia mwaka juzi, tuliwasilisha pia ombi la kutuondolea kodi kwenye Marupurupu

mbali mbaliyasiyo mshahara. Kwa heshima kubwa bado tunasubiri kusikia kauli yako kuhusiana na kulimaliza suala hili.

Kwa ujumla, tunaishauri serikali iweke utaratibu maalumu utakaoondoa makato ya kodi zaidi ya mara moja toka katika kipato cha mfanyakazi.Utaratibu unaotumika hivi sasa wa Mfanyakazi mmoja kukatwa kodi toka kwenye malipo ya mshahara, posho au marupurupu na likizo unapunguza kipato cha mfanyakazi.

6.3MAFAO YA WAFANYAKAZI

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa namna ya pekee kabisa, tunakushukuru sana kwa jinsi ulivyopokea na kushughulikia ombi letu la kuwalipa wafanyakazi wenzetu waliokumbwa na changamoto ya vyeti michango yao waliyochangia kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Zoezi hili limefanyika kwa moyo wa kizalendo sana hasa baada ya maombi kukamilishwa na waajiri na kuwasilishwa kwenye mifuko. Aidha, tunao wanachama wetu wachache ambao bado waajiri wao hawajatekeleza wajibu wao na hivyo hadi sasa baadhi yao hawajalipwa kama ilivyoelekezwa na serikali.

Tunashauri wafanyakazi walipwe michango yao na serikali iendelee kumaliza changamoto zilizopo na Waajiri ambao kimsingi hawakuwasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii baada ya kuwakata.

Aidha, jitihada zako zimeonekana dhahiri katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanaostaafu wanalipwa mafao yao kwa wakati bila kuchelewa. Ili kuiondoa kabisa changamoto hii, tunashauri mifuko ya hifadhi ya jamii ione uwezekano wa kuandaa mafao kwa wafanyakazi wanaoelekea kustaafu kwa kutumia mshahara wa mwezi wa mwisho kabla ya kustaafu kufanyia mahesabu ya mafao kwa mfanyakazi husika.

Mheshiwa Rais, ni mwaka mmoja umepita tangu uidhinishe Kanuni ya kikokotoo kipya na kuanza kutumika. Tathmini ya mwaka mmoja inaonesha kujaa kwa hofu kwa wafanyakazi zinazotokana na upotoshwaji mkubwa kuhusiana na jambo hili kutoka kwenye jamii na kwa baadhi ya wanasiasa. TUCTA tunaendelea kuishauri serikali kupitia Wizara ya Kazi kuendelea kutoa elimu sahihi kwa wafanyakazi juu ya suala hili. Tunaamini kuwa endapo uelewa utakuwa mkubwa kwa wafanyakazi inaweza kutupa picha halisi katika utekelezaji wake tofauti na jinsi ilivyo sasa.

6.4AFYA YA WANANCHI/WAFANYAKAZI

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Nia ya dhati ya serikali yako katika kuhakikisha kuwa afya za wanachi zinapewa kipaumbele imeonekana kwa vitendo. Kama nilivyosema hapo awali, ujenzi wa miundo mbinu ya kisasa, ununuzi wa vifaa na kuongeza wafanyakazi ni moja ya mifano kuthibitisha hilo.

Aidha; kuwepo kwa jitihada ya kuwa na Bima ya Afya kwa wote itatuhakikishia usalama wa afya zetu kwa kupata tiba sahihi na kwa wakati. Tunalipongeza Bunge letu kwa kazi kubwa na umakini wake katika kuhakikisha kuwa Muswada huu unapitiwa na kuleta malengo tarajiwa kwa watanzania.

Kwa sasa tunaendelea kushauri Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuboresha huduma zake hasa kwa watoa huduma wao ambao wamekuwa na malalamiko ya kucheleweshewa malipo ya huduma zilizotolewa na hivyo kushindwa kulipa haki za msingi za wafanyakazi ikiwemo mishahara. Kwa mazingira ya sasa ya sayansi na tekinolojia, hatutarajii kuona kuwa malipo kwa watoa huduma yanachelewa.

Pia, tunashauri kuwa katika mazingira ambapo mfanyakazi amekatwa michango ya 3% kwa ajili ya Bima ya Afya na Mwajiri hajawasilisha michango hiyo kwa mfuko kwa sababu zake, wafanyakazi wasinyimwe huduma kwani wao tayari wametimiza wajibu wao.

Mfuko uweke utaratibu ambao hautamuathiri mfanyakazi kwa makosa ya mwajiri wake kama ilivyo sasa. Wafanyakazi wengi pamoja na familia zao wameadhibiwa na kuathirika kwa kukosa huduma za afya kwa makosa ambayo kimsingi sio ya kwao.

6.5USHIRIKISHWAJI WA WAFANYAKAZI KATIKA UTATU

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Tumeendelea kushirikishwa katika maeneo mbali mbali ya kisheria yanayohitaji utatu kwa mujibu wa miongozo ya shirika la Kazi Duniani. Mabaraza ya wafanyakazi kwa sasa angalau yanafanyika kwa taasisi za umma na wafanyakazi tumeendelea kutoa michango yetu yenye tija kwa waajiri. Tunaendelea kutoa ushauri kwa waajiri wengi kuendelea kuitisha vikao walau viwili kwa mujibu wa Sheria.

Waajiri ambao bado hawaoni umuhimu wa vikao hivyo hasa kwenye Halmashauri zetu na baadhi ya Sekretaeti za Mikoa wasisitizwe kutekeleza wajibu huu wa Kisheria. Tushauri Zaidi kwa Serikali kuona uwezekano wa kuwa na Sheria zitakazowezesha mabaraza haya kufanyika pia kwenye sekta binafsi kwa kuwa mchango wake ni mkubwa kwa ufanisi wa kazi sehemu za kazi.

Katika kuendelea kutekeleza dhana ya UTATU, tunashauri sheria zetu za hifadhi ya jamii kutambua uwepo wa chombo kitakachokuwa na jukumu la kusimamia mifuko ya hifadhi ya

jamii. Hii itaondoa hali iliyopo sasa ambapo kuna idara tu iliyo chini ya Katibu Mkuu wizara ya kazi ambayo kimsingi dhana ya huu utatu haipo. Iliyokuwa SSRA ilifanya kazi yake kwa misingi ya utatu na pia kwa uhuru zaidi tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika kuhakikisha kuwa Ajira zenye staha zinapatikana kwa wafanyakazi wa sekta zote za umma na binafsi, tunatakiwa kuendelea kuimarisha usimamizi wa Sheria zinazosimamia utumishi katika sekta zote. Kama tulivyoainisha awali, wafanyakazi wanastahili haki na masilahi bora kwa kazi wanazofanya.

Aidha, wanatakiwa wawe na uhakika wa ajira zao hasa kwa kuwa na mikataba bora yenye kuwapatia uhakika wa ajira zao, malipo na haki ya hifadhi ya jamii na mazingira salama na yasiyoweza kuleta madhara ya kiafya kutokana na kazi zao.

Ili kuweza kufikia lengo hili muhimu, tunashauri serikali kuendelea kuimarisha Idara ya Kazi iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu: Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. Kwa hali ilivyo sasa tunatambua kuwa Idara hii inakabiliwa na changamoto kadhaa. Baadhi ya changamoto hizi ni kama upungufu wa Watumishi ambapo kuna wastani wa Maafisa kazi wawili kila mkoa,

upungufu vitendea kazi kama vile magari ya kuwawezesha kufika sehemu za kazi ili kufanya kaguzi kwa mujibu wa sheria. Changamoto hizo zinapelekea baadhi ya wafanyakazi wa kigeni kufanya kazi bila vibali, baadhi ya wafanyakazi kufanya kazi bila mikataba ya ajira, baadhi ya sehemu za kazi kutowapa wafanyakazi fursa ya kuunda matawi ya vyama vya wafanyakazi, hivyo wafanyakazi hao kukosa haki zao za msingi na kufanya kazi hatarishi na zisizo za Staha. Tunatambua kuwepo kwa miongozo na sheria zinasosimamia ajira za staha, lakini tunapokosa usimamizi madhubuti baadhi ya Waajiri huwanyima Wafanyakazi haki zao za msingi.

Aidha, tunapongeza jitihada za dhati kwa serikali kwa kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanalindwa na athari zinazoweza kutokea wanapokuwa kazini. Kama ilivyokuwa kwenye Idara ya kazi, tunashauri Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi (OSHA) waongezewe nguvu ya rasilimali watu na vifaa ili nao wafanye kaguzi za kutosha kwenye maeneo yetu ya kazi katika ofisi za umma na binafsi. Maeneo yetu ya kazi yakiwa salama, tutafanya kazi kwa furaha bila kuathiri afya zetu hata tutakapo staafu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika kikao cha Wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kilichofanyaka mwaka jana huko Geneva Uswisi kiliazimia kuwa suala ya usalama na afya mahali pa kazi liwe ni suala la

haki ya msingi kwa Wafanyakazi. Kwa maana hiyo Nchi Wanachama ikiwemo Tanzania walitakiwa kuhakikisha kuwa suala la usalama na afya kazini linapewa kipaumbele.

Sambamba na hilo Mheshimiwa Mgeni Rasmi tunakushukuru wewe binafsi pamoja serikali yako kwa kuanzisha mchakato wa kuridhia mkatataba wa Usalama na Afya wa ILO namba 155 kama ulivyosema katika sherehe za Mei Mosi kule Dodoma. Pamoja na juhudi hizi, tunakuomba pia uanzishe mchako wa kuridhia Mkataba wa ILO namba 187, unaohusu Nchi wanachama wa ILO kuweko Muongozo wa kuhamasisha masuala ya usalama na afya kazini kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya sehemu za kazi.

Kuridhia Mkataba huo ni moja kati ya vipaumbele vya nchi yetu na nchi wanachama wa ILO na SADC kama ilivyoamuliwa katika mkutano wa wanachama wa ILO na SADC uliofanyika hivi karibuni.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Nimalize kusoma risala hii ya Wafanyakazi kwa kukushukuru kwa mara nyingine kwa utayari wako wa kutusikiliza Wafanyakazi kila wakati tulipokuomba uwepo wako.

Tunakutakia kila la kheri na mafanikio katika jitihada zako za kuwaondolea Watanzania kero zinazowakabili na kuwaletea maendeleo wananchi wakiwemo kundi hili kubwa la Wafanyakazi.

Aidha, sisi kama Wafanyakazi, tunatumia fursa hii kuwaasa vijana na wananchi kwa ujumla kuendelea kujituma na kufanya kazi kwa weledi na uaminifu mkubwa. Imani tuliyopewa na viongozi wetu tuiishi kwa vitendo. Pia tuwaombe kuendelea kuishi kwa kuzingatia mila na desturi zetu bila kufuata mitindo ya maisha kinyume cha tamaduni zetu. Tunawaomba wazazi wote kushika nafasi zetu kikamilifu na kuwaeleza watoto ukweli na kuishi kwa kuzingatia maadili ya Kiafrika na pia kuzingatia mafundisho ya dini zetu. Naamini mmenielewa.